Ziada: - Anaweza kuwa kiongozi wa vijana, mwanasiasa, dini au sekta yoyote.
- Hadhira ni vijana wa Kikundi cha Mwangaza.

1. **Huu ni utungo wa kiuamilifu; hotuba. Vipengele vikuu vya utungo wa aina hii vidhihirike.**

**I. Muundo na mtindo**

Yafuatayo yazingatiwe:

(a) **Kichwa-** kitaje hatibu, wanaohutubiwa, na kiini cha hotuba

- Kutumia wakati uliopita.
- Kutoandika kichwa kabisa
- Asipozingatia itifaki ni kosa la mtindo
- Atumie alama za mtajo au asitumie ni kosa la mtindo
- Kikundi cha vijana ambacho si Mwangaza.
- Akitumia kaunti ambayo si Tazama mbele.
- Akikosa kutumia vijana katika maelezo yakini hoja zinalenga vijana.

Kutotumia vipengele vyote vinavyohitajika

(b) **Utangulizi**

Ubainishe:

-salamu/kuamkua hadhira

-kutambua wahusika kwa vyeo

-kujitambulisha

(c) **Mwili** –hoja zijadiliwe hapa.

(d) **Hitimisho** -Hatibu atoe muhtasari wa hoja/kiini cha hotuba, kisha awashukuru. Anaweza pia kutoa changamoto kwa hadhira.

- si lazima atoe muhtasari bali aonyeshe kutamatika kwa hotuba

(e) **Mtindo wa uwasilishaji wa hotuba uzingatiwe**

Utungo udhihirishe kuzungumza moja kwa moja na hadhira. Maswali ya balagha yanaweza kutumiwa kuchochea hisia za hadhira.

**II. Maudhui**

Hoja zijadiliwe katika mwili. Kila hoja ijadiliwe katika aya. Baadhi ya hoja ni:

(i) Vijana kuhusika katika utunzaji wa mazingira.

(ii) Kushiriki katika michezo mbalimbali ili kujiinua kibinafsi na kuinua uchumi wa kaunti.

(iii) Vijana watumie mapato yao kuwekeza kwa manufaa yao na ya kaunti.

(iv) Washiriki katika kilimo ili wakabiliane na changamoto ya kaunti kujitosheleza kwa chakula.

(v) Kuunda vikundi vya kusaidia kudumisha usalama; kila mmoja awajibikie kulinda usalama.

(vi) Kuwaelimisha wenzao kuhusu umuhimu wa kudumisha usalama katika kata na kaunti.

(vii) Washiriki katika harakati za kuelimisha umma kuhusu afya bora.

(viii) Kuhamasisha vijana wenzao na umma kuhusu umuhimu wa kudumisha maadili kama vile kukinga dhidi ya ufisadi, kutoshiriki matumizi mabaya ya vileo na ugaidi.

13. ~~Upanguzi wa~~ Uvumbuzi wa vipaji na nyumba ya kufanyia kazi mbalimbali
14. Kushiriki vikao vya kutoa maoni kuhusu maendeleo ya kaunti
15. Vijana kujiunga na vyuo vya kiufundi na kutumia ujuzi huo kuendeleza kaunti yao
16. Kupata elimu ya juu na kutumia ujuzi huo, wanapotafuta kazi katika kaunti yao
17. Kufanya utafiti kuhusu changamoto zinazokumba kaunti yao na kupendekeza suluhisho.



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Katika uchaguzi wa ... Wao kuwania viti vya uongozi katika kaunti yao.

(ix) Wasaidiane kutambua na kukuza vipawa kwa manufaa yao na kaunti/jamii kwa jumla.

(x) Wakuze uhusiano mwema baina ya wanajamii kupitia shughuli za kijamii kama vile kuandaa mashindano ya kandanda kwa vijana.

(xi) Waelimishane kuhusu umuhimu wa kukinga dhidi ya kufuata tamaduni zinazowarudisha nyuma, kwa mfano ndoa za mapema.

(xii) Kuanzisha na kujiunga na vyama vya ushirika ambavyo vitawapa mikopo ya kuanzisha miradi.

**9) Mtahiniwa anastahili kuandika insha ambayo inaonyesha manufaa ya kushiriki katika mazoezi ya viungo vya mwili.**

Baadhi ya hoja ni:

(i) Kuboresha afya/kuimarisha afya yao/afya yao itaimarika.

(ii) Wataweza kujiepusha na magonjwa yanayotokana na mienendo ya maisha.

(iii) Wataweza kujenga misuli yao.

(iv) Kuchangamsha ubongo na kuufanya utende kazi ipasavyo/kuimarisha utendakazi wa ubongo.

(v) Ni njia ya burudani/ kutuliza akili.

(vi) Kujenga ukakamavu/ujasiri.

(vii) Kuimarisha kujiamini na kujithamini.

(viii) Hujenga nafasi za ajira.

(ix) Hukuza vipawa.

(x) Huleta utangamano/ushirikiano baina ya watu.

(xi) Ni njia mwafaka ya kutumia muda wa ziada.

12. Kujipa sifa au umaarufu.
13. Kujenga mwonekano wa mwili
14. Kudhibiti uzani
15. Kujiepusha na kutenda maovu.
16. Kuongeza hamu ya chakula
17.

Tanbihi: Iwapo anasura aliyotenga na akose maudhui, atuzwe 4

**b) Mtahiniwa atunge kisa ambacho kinaonyesha hali ifuatayo:**

Mtu ambaye hutia bidii katika jambo (gumu) hatimaye hufanikiwa. Au mtu ambaye hujibidiisha kwa jambo katika mazingira magumu hatimaye huja kufanikiwa.

Hali zifuatazo zinaweza kujitokeza:

i) Mhusika ajiunge na shule ya upili apitie hali ngumu kama vile kukosa karo, sare, mavazi, kufiwa na mzazi/ugonjwa/masomo kuwa magumu ajizatiti na baadaye afanikiwe.

ii) Mfanyakazi aajiriwe, apitie magumu kama vile kubaguliwa, kunyanyaswa ...na aendelee kijibidiisha hatimaye apandishwe cheo.

**Tanbihi**

- Pande zote mbili za methali sharti zijitokeze. Aonyeshe kujibidiisha na kufanikiwa.
- Himiza bidii ama kuchanika
- Akitunga visa vingi, visa hivyo vioane na kisa kikuu
- Akitoa tu maelezo ni wa D)
- Kisa kikizuka kidogo ataenda C-
- Akishughulikia upande moja hatapita 10/20
- Anabidii na afaulu — Amejitungia
- Maadili yazingatiwe.



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

C

**Hii ni insha ya mdokezo**

(i) Ni insha ya masimulizi. Mtindo wa kimasimulizi utumiwe.

(ii) Mtahiniwa atunge kisa ambacho kinaoana na utangulizi/mwanzo uliotolewa.

(iii) Ruwaza ifuatayo inaweza kujitokeza:

- Mhusika alikuwa amepitia hali ngumu, akafanya uamuzi/akachukua hatua kwa madhumuni ya kubadili hali hiyo.

**Tanbihi**

i) Baada ya kauli, mtahiniwa anaweza, ama kuendeleza kisa, akasimulia yaliyotokea au akaturudisha nyuma (mbinu rejeshi) akatuhadithia yaliyomfanya mrejelewa kuamua kuchukua hatua.

ii) Kisa kinaweza kuendelezwa kwa nafsi ya tatu, nafsi ya kwanza au mchanganyiko wa nafsi.

iii) Hatua inayochukuliwa ~~sharti~~ isababishe matokeo mazuri/ imwondolee mhusika dhiki/changamoto alizopitia. au inaweza kutoleta afueni.

iv) Si lazima matokeo yawe mazuri, yanaweza kuleta hasara, madhara au matokeo mabaya.

— Baadaye, nilipata nafasi ya kwenda ughaibuni.

- Anaweza kutumia mbinu rejeshi
- Mhusika awe na matumaini
- Matumaini yake yanaweza kufaulu.
- Kisa kioane na mdokezo ila anaweza kutosa kutumia mdokezo kwa vyovyote vile,
- Mdokezo unaweza kutumika mwisho — Mtindo.

- Changamoto
- Hatua iliyochukuliwa
- Afueni | hasara



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes